



Our Mission

To improve uptake of Ante-Natal Care (ANC) visits and promote safe deliveries in health facilities for every mother.

To give every child born a dignified start to life.



Website: totobox.org



Toto Care Box

Mwongozo kwa
mama mjaa mzito



**Heshima ya Mwanzo
ya Maisha**

(A Dignified Start to Life)

Niamey Lane
Sumba Road, Nairobi West
Nairobi, Kenya.

Phone: 0719313712

E-mail address: totocareboxltd@gmail.com

Website: totobox.org

Mpango binafsi wa kujifungua salama

Andaa, zungumza na mwenzako, jaza mpango.

- Tembelea kituo cha kutoa huduma za afya. Hakikisha umeenda hicho kituo mara NNE kabla ya kujifungua.



- Fahamu tarehe ya kujifungua.



- Unapojifungua kwa kituo cha huduma cha afya, utapewa **Toto Care Box** itakayo kusaidia kuanza kulinda mtoto wako.

Dalili za hatari kabla ya kujifungua /wakati wa kujifungua/baada ya kujifungua

- Kutoka damu kwenye sehemu ya mkojo.
- Kuumwa sana na kichwa na kuona maluweluwe/kushindwa kuona na kizunguzungu.
- Kupoteza fahamu au mtukutiko wa mwili /kifafa cha mimba.
- Kuchoka haraka, kupumua kwa shida.
- Homa.
- Mtoto kuacha kucheza tumboni.

Toto Care Box

Vifaa vilivyo kwenye kijisanduku cha Toto Care Box.



ILANI!!

USIFUNIKE MTOTO AKIWA NDANI YA TOTO CARE BOX.

Dalili za hatari kwa mtoto:

1. Mtoto anashindwa kunywa au kunyonya.
2. Mtoto anatapika kila kitu.
3. Mtoto anadegedege.
4. Mtoto anapoteza fahamu.
5. Mtoto ana joto.
6. Mtoto hakojo.
7. Mtoto hajaenda choo kikubwa siku mbili.
8. Mtoto anahema kwa haraka.
9. Mtoto anatoa sauti akihema.
10. Kitovu kinatoa usaha au damu.
11. Ngozi ya mtoto na macho yanabadilika na kuwa rangi ya manjano.
12. Mtoto anakosa kutulia na anashinda akilia.
13. Mtoto anaendesha na kutapika.

Mapendekezo

- Hakikisha umemnyonyesha mtoto wako kwa **nusu saa anapozaliwa.**



- Hakikisha umemnyonyesha mtoto wako kwa **miezi sita mfululizo.**
- Hakikisha umepata masomo ya **lishe bora, huduma ya kwanza, mpango wa uzazi** na **usafi binafsi** kwenye hospitali.